

TAARIFA FUPI YA MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI KUFIKIA TAREHE 17/09/2020.

1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ni mojawapo ya **Halmashauri nane** zilizopo katika Mkoa wa Mwanza ambayo ilianzishwa tangu **mwaka 1995** baada ya kugawanywa kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ambayo mwaka **2018/2019** ilipata fedha kutoka Serikali kuu za kuanzisha utekelezaji mradi wa ujenzi wa Jengo la Halmashauri.

Mradi huu wa ujenzi wa Jengo la Halmashauri unaendelea vizuri chini ya Mkandarasi ambaye ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na usimamizi wa Wataalam na Wahandisi wa Mkoa na Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ambapo ujenzi umefikia asilimia **70** ya utekelezaji.

2.0 GHARAMA YA MRADI

Gharama ya mradi huu inakadiriwa kutumi kiasi cha **Tshs 2,900,000/=** kwa mujibu wa Mkataba hadi kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo litakalokuwa na ofisi za kutosha Watumishi wa Idara na Vitengo vyote vya Halmashauri.

3.0 HATUA YA UTEKELEZAJI WA MRADI.

Mradi huu upo hatua ya ukamilishaji na fedha zilizotumika hadi sasa zinakadiriwa kufikia **Tsh, 1.5 (Bilioni 1.5)** ambayo ni sawa na asilimia ya ujenzi ambapo kwa sasa tayari Jengo la ghorofa moja limezekwa na kupigwa lipu na mashimo ya choo yamechimbwa na kufunikwa, maandalizi ya kuweka vigae, bodi, kuweka madirisha ya vioo na milango yanaendelea pamoja na kupaka Rangi ndani na nje, kuweka miundombinu ya umeme na maji, na miundombinu ya mifumo ya TEHAMA.

Nawasilisha,

Anna Urio
Kny. Mkurugenzi Mtendaji (W)
MISUNGWI

PICHA HAPA CHINI, IKIONYESHA MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI UPO KATIKA HATUA YA UKAMILISHAJI NA MAANDALZI YA KUWEKA VIOO NA MILANGO YANAENDELEA.



PICHA HII, IKIONYESHA MWONEKANO WA NAMNA JENGO LA GHOROFA MOJA LA OFISI ZA HALMASHAURI YA MAISUNGWI NA UJENZI UNAENDELEA KWA KASI.



PICHA CHINI IKIONYESHA UPANDE WA MBELE WA JENGO LA HALMASHAURI NA NAMNA UJENZI UNAVYOFANYIKA KWA KASI

